JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI, TEKNOLOJIA NA UFUNDI

SHULE YA SEKONDARI
KANTALAMBA,
S.L.P. 70, SIMU: 025-2802017,
SUMBAWANGA.

Kumb. Na.
J/KSS/2/65

TAREHE: .....

MWANAFUNZI .....

S.L.P. .....

.....

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE HII MWAKA 2018.

Ninayofuraha kukufahamisha kwamba umechaguliwa kujiunga na Shule hii katika kidato cha Kwanza (I) mwaka 2018. Ninachukua nafasi hii kukupongeza kwa jitihada zako zilizowezesha kustahili uchaguzi huu. Ni tegemeo langu kwamba jitihada hizo utaziongeza uwapo katika shule hii. Shule ya Sekondari Kantalamba ipo katika Manispaa ya Sumbawanga. Manispaa hii ambayo ni makao Makuu ya Mkoa wa Rukwa ipo umbali wa kilometa 336 toka Mbeya na kilometa 240 toka Mpanda. Upo usafiri wa uhakika kila siku toka Mbeya ambapo mabasi huondoka kuanzia saa 12:30 alfajiri na kuwasili Sumbawanga saa 7.00 mchana. Kutoka Mpanda usafiri upo kila siku ambapo gari huondoka saa 1:00 Asubuhi na kuwasili Sumbawanga saa 7:00 mchana, shule ipo umbali wa kilometa tatu (3). Kwa kutumia usafiri wa taxi utalipa shs. 4,000/= tu na kwa kutumia mabasi madogo (dala dala) utalipa shs. 400/= tu. Muhula wa kwanza wa masomo utaanza 08.01.2018 unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia 08.01.2018 na mwisho wa kuripoti ni 29.01.2018.

Yafuatayo ni maagizo na mahitaji muhimu ambayo utatakiwa kuyatimiza kabla ya kujiunga na shule hii.

MAMBO YA MUHIMU YA KUZINGATIA.

A: SARE YA SHULE:

(i) **SURUALI 2 DARK BLUE**: Zenye malinda mawili kila upande na mkunjo au pindo chini (turnup) na isiyobana chini.

(ii) **SURUALI 2 RANGI YA KAKI:** Zenye malinda mawili kila upande na mkunjo au pindo chini (turnup) na isiyobana chini.

(iii) **SURUALI 1 RANGI YA NJANO: Yenye malinda mawili kila upande na mkunjo au Pindo juu. (tunup)**

(iv) **SHATI 2 RANGI NYEUPE:** Mikono mirefu lenye mfuko mmoja kifuani upande wa kushoto.

(v) **VIATU:**

- **Rangi** nyeusi vyenye kamba, visiwe na soli nene, hairuhusiwi kuvaa viatu vya matairi,
- Kandambili au yeboyebo wakati wa masomo darasani na bwaloni / ukumbi wa chakula.

(vi) **SOKSI;**

- Rangi nyeupe isiyo na urembo wowote.

(vii) **MKANDA:**

- Rangi nyeusi na uwe wa ngozi

(viii) Usiwe na madoa au urembo wowote

(ix) **T. SHIRTS:**

- Rangi ya kijivu yenye kola na nembo ya shule itapatikana shuleni kwa Tsh. 12000/=

- Rangi ya dark blue yenye kola na nembo ya shule itapatikana shuleni kwa Tsh.12000/=

(x) SWETA:

- Rangi ya blue

(xi) NGUO ZA MICHEZO:

- Unatakiwa uje na nguo za michezo, bukta na fulana (zote rangi nyeusi) na track suti (lightblue) rangi nyeusi.
- Uje na Raba kwa ajili ya michezo.

NB. Ili kuondoa usumbufu wa kutofatiana kwa rangi na mshono, mzazi Anashauriwa ashonee suruali sumbawanga.

1. VYOMBO VYA CHAKULA:

- Nunua vyombo vya chakula ambavyo ni sahani, bakuli, kikombe pamoja na kijiko.

2. VIFAA VYA USAFI:

- Uje na ndoo ya lita kumi (10) kwa ajili ya usafi binafsi.
- Uje na ufagio aina ya chelewa kwa ajili ya usafi wa mazingira.
- Uje na jembe lenye mpini.
- Uje na drier
- Uje na ndoo ya lita 20 kwa ajili ya kuchotea maji ya jikoni.
- Uje na fyekeo.

3. MAGIZO MENGINE.

- Uje na godoro futi 2 ½
- Chandarua, mashuka mawili blue bahari
- Taulo, blanketi na Sanduku la chuma (Tracker)
- Uje na Copy ya cheti cha kuzaliwa.
- Madaftari ya kutosha (counter books 12) na vitabu.

4. FEDHA ZA MATIBABU NA MATUMIZI.

- Unashauriwa uje na fedha ya matumizi madogo madogo kama vile kununua sabuni, mafuta n.k. na gharama za matibabu.

5. LIKIZO ZA MIHULA.

- Mwezi wa **Juni na Disemba** hakuna mwanafunzi anayeruhusiwa kubaki shuleni wakati wa likizo.

B. SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE HII.

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa Sheria Na. 10: ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi, yenye dhamana ya elimu nchini na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji Elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni.

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.
iii. Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (preparation).
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule.
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa.
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote, na
ix. Kutunza mali za umma.

C. Makosa yafuatayo yanaweza kusababisha kufukuzwa au kusimamishwa shule.

i. Wizi
ii. Uasherati na ushoga.
iii. Ubakaji.

iv. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kubeli na kadhalika.
v. Kupigana au kupiga.
vi. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
vii. Kudharau Bendera ya Taifa.
viii. Kuwa mjamzito / kupata mimba.
ix. Kuoa au kuolewa.
x. Kutoa mimba.
xi. Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.
xii. Kukataa adhabu kwa makusudi
xiii. Kuwa na simu ya mkononi.

SHULE YA SEKONDARI KANTALAMBA

FOMU YA KUANDIKISHWA SHULENI NA HABARI ZA MZAZI WA MWANAFUNZI

A: HABARI ZA MWANAFUNZI.

Jina kamili kama alivyoandikishwa kwenye mtihani.

1. **----------**
2. **Tarehe ya kuzaliwa: ----------**
3. **Dini: ----------**
4. **Uraia: ----------**
5. **Shule uliomaliza: ----------**
6. **Uje na cheti cha kuzaliwa:**
7. **Uje na results slip na Leaving certificate (Original).**

B: HABARI ZA MZAZI.

1. **Jina kamili: ----------**
2. **Kazi yake: ----------**
3. **Mahali pa kazi: ----------**
4. **Dini: ----------**
5. **Uraia: ----------**
6. **Wilaya ya Nyumbani: ----------**
7. **Maelezo mafupi kuhusu afya ya mwanafunzi: ----------**

   ----
8. **Ninathibitisha kwamba taarifa zilizotolewa hapo juu ni kamili na kweli.**
9. **Anuani ya Nyumbani: ----------**

Sahihi ya Mzazi / mlezi

3

SHULE YA SEKONDARI KANTALAMBA
FOMU YA KUKIRI KUKUBALI SHERIA ZA SHULE.

A: SEHEMU YA MWANAFUNZI.

JINA LA MWANAFUNZI ----------

TAREHE YA KUZALIWA ----------

UHUSIANO (UNDUGU) NA MLEZI, (BABA, MJOMBA, KAKA)

KIAPO CHA UTII:

MIMI ----------
Nikiwa mwanafunzi wa Shule hii nakubali kuwa, umma wa nchi hii ya Tanzania ndiyo ulionipa nafasi hii maalumu ya masomo, ili nimalizapo niweze kuitumikia nchi katika Maendeleo yake.

Hivyo basi ninaahidi kwamba, nitajibidisha hapa shuleni na pia nimalizapo shule. Ili kutimiza shabaha hiyo ninakubali na kuahidi kwa hiari yangu mwenyewe kuwa nitatii sheria za shule na amri zote nitakapopewa na walimu wangu.

Nikiwa na malalamiko au maoni nitayafikisha kwa viongozi wa shule kufuatana na utaratibu uliowekwa bila ya kuogopa chochote. Nitakuwa tayari kuchukuliwa hatua za kinidhamu zinazostahili iwapo nitakuwa nimekiuka sheria za shule.

Sahihi ya mwanafunzi ---------- Tarehe ----------

SEHEMU YA MZAZI/MLEZI.

Mimi ---------- ambaye ni mzazi/mlezi wa mwanafunzi mtajwa hapo juu, naahidi kutoa ushirikiano mzuri na uongozi wa shule katika kumlea mwanangu. Hii ikiwa ni pamoja na kutomnunulia simu ya mkononi mwanangu. Nitakuwa tayari kushirikiana na uongozi wa shule katika suala la nidhamu ya mwanafunzi na kwamba nitakuwa tayari kukubaliana na adhabu itakayotolewa iwapo mwanafunzi atakuwa amehusika na utovu wa nidhamu.

Sahihi ya mzazi/mlezi ----------
Namba ya simu ya mzazi/mlezi ----------
Tarehe: ----------

Tafadhali soma kwa makini maelezo / maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

KARIBU SANA KATIKA SHULE HII.

MKU WA SHULE

4.

MINISTRY OF EDUCATION SCIENCE, TECHNOLOGY AND VOCATIONAL TRAINING

KANTALAMBA SECONDARY SCHOOL,
S.L.P. 70,
SUMBAWANGA,
RUKWA.

MEDICAL OFFICER:

REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION.

Please examine the above named as to His/Her fitness to is/her fitness as indicated below, arrange for necessary treatment so that the certificate may be signed and brought to school by the student.

This certificate must be signed by a qualified Medical Officer of recognized hospital.

MEDICAL CERTIFICATE.

I have examined the above named student with regard to:

Skin: ----------

Eyes: ----------

Teeth: ----------

Spleen: ----------

Abdomen: ----------

-

Urine: ----------

-

Hemoglobin: ----------

--

Chest: ----------

--

Any Disabilities: ----------

I consider that: ----------

He/She is in good health free from infections diseases, and fir to come to school

He/She is fit to come to school after having: ----------

Treatment for: ----------

She/is not pregnant.

Date: ---------- **----------**

MEDICAL OFFICER